Swahili

Je bado hujaajiriwa kazi

Je una uwezo mwingi

Je ungependa kuanza biashara yako

Kujitayarisha Kuanza biashara

Udhamini kwa Wakimbizi Watendaji
Muongozo wa Wakimbizi

rib
REFUGEES INTO BUSINESS

Refugees into Business
© The Prince's Trust and the Refugee Council 2006

This booklet is for guidance only.

This project is funded by the Phoenix Fund and the Small Business Service of the Department of Trade and Industry.

This booklet is also available in the following languages: Amharic, Arabic, Dari, Farsi, French, Pushto, Kurdish Sorani, Portuguese, Somali, Swahili, Tigrignia and Turkish.

Refugees into Business is a project managed by Refugee Enterprise Partnership, lead by the Refugee Council.

The Refugee Enterprise Partnership consists of the British Refugee Council, Refugee Action (RA), Refugee Women's Association, Social Enterprise London, the Prince's Trust, Community Action Network, and Education Action International.

With thanks to the Language and Literacy Unit+ (LLU+), London Southbank University, who has helped ensure the text is accessible to people who are at least at entry level 3 in their reading of English.

www.refugeesintobusiness.org.uk/translated_ten_steps

© The Prince's Trust and the Refugee Council 2006

Supported by PHOENIX FUND

Yaliyomo

Kujitayarisha Kuanza biashara

Hapa kuna hatua kumi zitakazo kusaidia unapojitayarisha kuanzisha biashara yako.

1. Kuwa na imani. 3
2. Hakikisha kwamba unaruhusiwa na sheria kuanzisha biashara yako. 5
3. Tayarisha muhtasari wa stakabadhi zako za ujuzi na masomo uliyomaliza na kutimia pamoja na historia ya kazi ulizofanya (C.V). 8
4. Pata usaidizi ili uweze kuimarisha kiingereza chako. 11
5. Pata mafundisho kuhusu kufanya biashara. 14
6. Jitolee kufanya kazi katika biashara ndogo iliyokaribu nawe au pia jitoloee kusadia katika Jamii. 16
7. Panga vile watoto wako watachungwa ukiwa kwenye biashara au masomo. 18
8. Panga matumizi ya pesa zako. 20
9. Pata usaidizi kutoka kwa watalamu katika kuanzisha baishara yako. 23
10. Mahala pengine pa kupata usaidizi. 26

© The Prince's Trust and the Refugee Council 2006

Hatua 1: Kuwa na imani

Wakimbizi na wahamiaji wamekuwa wakija Uingereza kwa mamia ya miaka huku wakileta faida kwa itikisadi ya Wawingereza. Baadhi ya biashara na mawazo zao zimesitawi sana na sasa zimekuwa ndio mtindo wa maisha ya kila siku.

Kwa mfano ulijua kwamba…?

→ Utamaduni wa 'samaki na chips' uliletwa na wahamiaji. Bwana Joseph Malin kutoka Mashariki ya Bara Ulaya ndiye aliyefunguwa biashara ya kwanza ya aina hii upande wa London mashariki, mwaka wa 1860.

→ Bwana Deloitte, mkimbizi kutoka kwenye mzunguko wa Ufaransa alipata kufika mjini Hull zaidi ya miaka 200 iliyopita. na kuanzisha biashara ya kuhusu hesabu. Mjukuu wake aliweza kuifanya biashara ile kuwa biashara mojawapo kubwa nchini na hivi sasa biashara hiyo ni Deloitte na Touche inayojulikana ulimwengu mzima.

→ Bwana Alec Issigonis, mkimbizi kutoka Uturuki, alifika Uingereza pamoja na familia yake mwaka wa 1922. Mtengezaji wa magari, aliyapenyeza duniani Magari ya uingereza ya aina; 'Morris Minor' na 'Mini'.

Marks & Spencer

Bwana Michael Marks alizaliwa Slonim, Urusi, mwaka wa 1859. Akiwa angali kijana, Marks alihamia Uingereza. Hakuwa na ujuzi wowote na pia hakuweza kuongea kiingereza. Alihamia hadi mji wa Leeds na kupata kazi katika kampuni iitwayo Barran iliyo waajiri wakimbizi. Hatimaye, Marks alikuwa amehifadhi pesa za kutosha kuanzisha kibanda katika soko la wazi mjini Leeds. Kando ya kibanda chake alikuwa ameweka kibao kilichoandikwa; "Usiulize Bei, ni peni moja tu". Kwa miaka iliyofuatia Marks alifungua vibanda vya aina hii katika soko nyingi mjini Yorkshire na Lancashire.

IKatika mwaka 1894, ilimbidi Marks kutafuta mshiriki ili aweze kueneza biashara yake. Na hapo ndipo Tom Spencer aliungana naye. Spencer alikuwa akifuata kwa makini Maendeleo ya Marks katika biashara. Kwa hiyo, alikubali kumpa Marks pauni mia tatu (300)

ili apate kumiliki nusu ya kampuni iliyokuwa ya Marks. Kati yao waliamua, Spencer atasimamia ofisi na maghala, Marks ataendelea na shughuli za kupanua masoko. Kupitia usaidizi wa Tom Spencer, Marks aliweza kufungua maduka huko Manchester, Birmingham, Liverpool, Middlesbrough, Sheffield, Bristol, Hull na Cardiff.

Kufikia 1897, Marks & Spencer ilikuwa biashara kubwa ikiwa na maduka Thelathini na sita (36). Katika mwaka wa 1903, Marks & Spencer ikafanywa kampuni na Tom Spencer alistaafu baadaye mwaka huo akiwa ametajirika kweli. Michael Marks aliendelea kuijenga biashara na kufikia kifo chake tarehe 31 Disemba, 1907 aliwacha biashara iliyokuwa na fahari sana kote Uingereza.

Haijalishi kama biashara yako ni kubwa au ndogo, iwe ni kibanda katika soko au kampuni iliyoshughulika na hesabu, inaweza kufanikiwa. Una kila haki ya kujaribu kwasababu ikifanikiwa, sio wewe tu utafanikiwa, bali pia Jamii yote. Hata hivyo, ni vizuri ujishughulishe na ufahamu matatizo unayoweza kuyapata wakati unapoanza biashara yako. Unapaswa kufikiria kwa hadhari mawazo yako na ujuzi wako kabla ya kuanza biashara kwa maana sio kila mtu anafaa kujiajiri kazi. Mwongozo huu utakusaidia kukumbana na haya na itakutambulia mahala pa usaidizi.

→ Kutoka mashirika yanayo jihusu kutoa msaada wa kwanza kwa biashara.
→ Hadi marafiki, familia na Jamii ambao unaweza kuwauliza mawaidha.

Utahitaji kutumia tegemeo za aina yote zipate kusaidia biashara yako kufanikiwa.

Kile unachoweza	Kile usichoweza
Tafadhali UNAPOSOMA taarifa hii, andika majina ya watu na mashiriki yote ambayo yanaweza kukusaidia na sehemu tofauti tofauti za biashara yako.	USIFIKIRI kwamba uko peke yako. Kufanikiwa kwa biashara yako kutakutegemea wewe, lakini pia kuna usaidizi mwingi pande zote za kukusaidia.

© The Prince's Trust and the Refugee Council 2006

Hatua 2: Hakikisha kwamba unaruhusiwa na sheria kuanzisha biashara yako

Sheria za nchi zinasema kwamba unaruhusiwa kuanzisha biashara yako kama Una:

→ Ruhusa ya kufanya kazi na kuondoka au una ruhusa ya kuishi nchini na kuondoka. Ruhusa ya kuishi Uingereza inaweza kupatikana kwa njia tofauti:

1. Kama umepewa kibali cha mkimbizi

i. Kabla ya Mwezi wa Nane 2005, kama ulipata kibali cha mkimbizi utaweza kupata ruhusu isiyodhihirika ya kubaki Uingereza (Indefinite Leave to Remain) (ILR) na kwa hiyo kuweza kuishi Uingereza Kabisa.

ii. Kama ulipata kibali chako cha Mkimbizi baada ya mwezi wa Nane, 2005, ruhusu yako ya kubaki ni ya wakati – miaka 5. Kesi zitaangaliwa baada ya miaka mitano, na kama bado kuna shida nchini uliotoka basi utaweza kuongezewa muda au kupata ruhusa isiyodhihirika ya kubaki Uingereza, kama sivyo basi utaweza kuhamishwa na kurudishwa nchi uliyotoka.

2. Ruhusa ya muda kuingia Uingereza na kuishi kule, ama yoyote

i. Ulinzi wa Kibinadamu (Humanitarian Protection): (Kabla ya mwezi wa nane 2005, hii inapela kwa muda wa miaka mitatu. Kuanza Mwezi wa Nane, 2005, ruhusa inaweza kuwa ya miaka mitano (5). Kesi yako itaangaliwa tena baada ya muda huu. Kama bado kuna shida nchini ulikotoka unaweza kuongezewa muda wa ulinzi au ILR. Kama hakuna shida yoyote basi itabidi urudishwe nchini mwako) Ama:

ii. Ruhusa maalum ya kuishi nchini (Discretionary Leave to Remain) . (Ruhusa hii hupewa kwa muda wa miaka mitatu (3) au muda chini ya miaka mitatu. Kuanzia mwezi wa Nane, 2005, kesi zitaangaliwa tena baada ya miaka mitatu na labda utapata

kuongezewa muda au hautaongezewa. Ikikubaliwa kwamba huhitaji ulinzi, unaweza kurudishwa nchini kwako. Unaweza pia kupata ILR kama utakubaliwa kubaki nchini Uingereza kwa miaka mingine sita (6)).

Kumbuka: Ruhusa rasmi za kuishi kwa muda au kuishi kabisa, zina ruhusu kwamba unaweza kufanya kazi na kupata faida za kijamii kama mwingereza.

Utajua aje kwamba una ruhusa ya kufanya kazi na kuishi Uingereza. Angalia:

→ Stakabadhi zako za uhamiaji au
→ Barua rasmi iloyotoka Ofisi ya Mambo ya Ndani (Home Office) inayokupa ruhusa hii kuishi Uingereza.

Stakabadhi hizi zitakueleza kama una ruhusa ya kufanya kazi na pia muda ulio nao kuishi Uingereza. Kama muda wako uko Karibu kuishi basi tunakushauri kurekebisha hali hii kabla ya kuanza biashara yako. Unaweza:

→ Kuwasiliana na mashirika yaliyopewa hapa ili kupata usaidizi. Watakuelezea cha kufanya.
→ Andika barua kwa Ofisi ya Uhamiaji kuhusu hali yako
→ Pigia simu Ofisi ya Mambo ya Ndani ili upate kujua muda ambao itawachukua kuidhinisha hati yako ya maombi.

Mara tu unapopata ruhusa rasmi ya kukaa, basi anza kufikiria jinsi utakavyo anzisha biashara yako.

© The Prince's Trust and the Refugee Council 2006

Kile unachoweza	Kile usichoweza
JARIBU kuhakikisha kwamba una muda wa miaka mitatu (3) ambapo unaweza kuishi Uingereza. Hii itakuwezesha kupata mkopo wako na kuanzisha biashara yako kabla tena kuanza kushughulikia na mambo ya uhamiaji.	USIJARIBU kuanzisha biashara yako wakati muda wako wa kuishi Uingereza uko Karibu kuisha. Itakuwa vigumu kupata usaidizi wa kuanzisha biashara yako katika hali hii. Hata zaidi huwezi kupata mkopo wa kuanzisha biashara yako.

Unaweza kupata taarifa zaidi hapa:

Kama una maswali kuhusu hali yako ya uhamiaji unaweza kuangalia hapa:

- → Baraza la Wakimbizi (Refugee Council) www.refugeecouncil.org.uk
- → Huduma ya Uhamiaji (Immigration Advisory Service) www.iasuk.org.uk
- → Kituo Cha Sheria kuhusu Wakimbizi (Refugee Legal Centre) www.refugee-legal-centre.org.uk
- → Idara ya Wakimbizi Nchini (Immigration Nationality Department) www.ind.homeoffice.gov.uk
- → Kituo cha Ushauri kwa Wananchi (Citizens Advice Bureau) www.adviceguide.org.uk/index/your_rights/immigration
- → Ukumbi wa Wafanyikazi (Employability Forum) www.employabilityforum.co.uk

Hatua 3: Tayarisha muhtasari wa stakabadhi zako za ujuzi na masomo uliyomaliza na kutuma pamoja na historia ya kazi ulizofanya (C.V)

CV(Curriculum Vitae) ni rekodi ya pahala ambapo umefanya kazi na masomo uliyopokea. Hapa Uingereza kila mtu anatayarisha CV wakati anatafuta kazi au usaidizi wa kuanzisha biashara. Pata hapa mifano za kuandika CV yako.

Unaweza kuwa na ukosefu hapa na pale katika masomo na kazi yako. Hii haijalishi, kama unaweza kuonyesha CV yako, na kama una ujuzi waq kuanza biashara kama vile vya kuweka hesabu, ujuzi wa soko, ujuzi wa kuamuru na kuongoza watu na kadhalika.

Unaweza kupata msaada kutoka:

- → Marafiki na jamiiambao wameandika CV's zao.
- → Mashirika yanayo peana mawaidha kuhusu mwendo, lakini kuna uwezekano kwamba utalipia huduma hii.
- → Balozi za wakimbizi au za kujitolea bila malipo zinaweza kupeana mawaidha ya bure.

Historia ya masomo
Andika kuhusu elimu, (shule, vyuo vikuu, au chuo kikubwa) pia/au malezi. Andika sifa yoyote ile uliopata ukifuata orodha ya wakati.

Wakati mwingine utapata kuitishwa vyeti kuthibitisha uwezo wako:

- → **Kama una vyeti** vyako na ungependa uwezo wako kutoka nyumbani vitambuliwe huko Uingereza, Taasisi ya Utathmini wa Taarifa nchini Uingereza (National Recognition Information Centre for the United Kingdom) (UK NARIC), itakupatia huduma hii. Utapaswa kuonyesha vyeti vyako na inaenda ikawa utalipa.

© The Prince's Trust and the Refugee Council 2006

→ **Kama huna vyeti** vya sifa yako, basi andika historia yako ya masomo na mawaidha uliyoyapata kutoka kwa mashirika ya usaidizi wa kuanza biashara. (hatua 9) iendapo utaitishwa vyeti.

NB: Huku historia ya masomo itasaidia, usitie shaka kama una sifa kidogo, ni ujuzi wako wa biashara ambayo itawapendeza balozi wa kusaidia kuanza biashara..

Historia ya Kazi

Andika orodha ya kazi ulizowahi kufanya ukianza na ya mwisho hadi ya kwanza. Pia andika zile shughuli ambazo ziliambatana na kila kazi. Hii itakuwa historia yako ya kazi. Itaonyesha kama una ujuzi wa kuanzisha biashara. Kama una ujuzi wa kibiashara kutoka hapo awali, basi tilia maanani ujuzi huo unapotayarisha historia yako ya kazi.

→ Nchini Uingereza utahitaji kupatiana kumbukumbu kutoka kwa waamuzi wawili. Kumbukumbu ni barua fupi inayoandikwa na muajiri wako wa mwisho ambayo inatoa ushahidi kuhusu uwezo na maarifa yako.
→ Wakati mwingine inakuwa vigumu kama muajiri wako wa hapo awali yuko nchi nyingine ama iendapo ni vigumu kuwasiliana naye. Njia moja ya kupata ujuzi unaopaswa na pengine kupata kumbukumbu ni kujitolea kufanya kazi kwenye biashara iliyo katika jamii. (Angalia chini na hatua 6).
→ Kama kuna pengo katika historia yako ya kazi, pata ushauri (angalia hatua 9) wakati unaposaka msaada kutoka shirika la kusaidia kuanzisha biashara.

Kazi za Kujitolea

Taarifa ya kazi yoyote uliofanya bila malipo pia ni muhimu. Kwa mfano kufanya kazi kwa nia ya kusaidia jamii ya ndani au kufanya katika biashara, itasaidia kuonyesha ujuzi wako binafsi.

Kile unachoweza	Kile usichoweza
ANDIKA kila jambo ambalo umefanikiwa kufanya. Fikiria pia vile ambavyo unaweza kumfanyia mtu kazi bila malipo. Baadaye unaweza kuwauliza wawe wadhamini wako.	USITIE shaka kama huwezi kuonyesha historia yako ya masomo au kazi. Hii ni hali inayowakumba wakimbizi wengi.

Unaweza kupata taarifa zaidi hapa:

→ Taasisi ya ndani zaidi (Jobcentre Plus), hupeana mawaidha kadha kuhusu kujiajiri kazi na inaweza kusaidia kukuonyesha njia ya kupata msaada wa CV www.jobcentreplus.gov.uk
→ Intaneti hupeana mitandao mengi yanayo peana msaada bure wa vile kuandika CV kama vile BBC www.bbc.co.uk/radio1/onelife/work/index.shtml?cvs/ or www.workthing.com or http://jobsadvice.guardian.co.uk/
→ Vyuo vikuu mara nyingi pia wana mawaidha ya kuandika CV's kwenye vitandao vyao.

© The Prince's Trust and the Refugee Council 2006

Hatua 4: Pata usaidizi ili uweze uimarishe kiingereza chako

Unapaswa kuwasialina vyema katika lugha ya kila siku na ya biashara. Hii ina faa kwa mfano:

→ Kuandika ramani ya biashara yako.
→ Uweze kushauriana na yule atakukopesha pesa au kujiandikisha kupata Ushuru (Value Added Tax (VAT)).

Ni muhimu upate kuelewa ni nini haswa huendelea kwenye kila sehemu ya biashara yako.

Mahala pa kupata usaidizi
Masomo ya kiingereza sana sana huitwa Kiingereza ya Wanenaji wa lugha zingine, (Speakers of Other Languages (ESOL)). Mpaka mwezi wa nane 2007, ESOL ni bure kwa wakimbizi na wanaosaka kimbilio. Baada ya mwezi wa nane 2007:

→ Kama una **ruhusa ya kubaki** (leave to remain) (hiyo ni, cheo cha mkimbizi, ulinzi wa huruma au ruhusa ya kutanadhari (discretionary leave)) kama huja ajiriwa na unapata ufanisi unastahilishwa kupata msaada wa ESOL bure.
→ **Lakini wanaosaka kimbilio la hifadhi na walio zaidi ya umri wa kumi na tisa (19)** wanapaswa **kulipa** masomo ya kiingereza. Kuna weza kuwa na mashirika mahali maalum yanayo peana masomo ya bure au ya bei nafuu.

Maktaba ya mtaa, balozi ya wakimbizi, Job Centre au Learndirect zitakupatia taarifa kuhusu mashirika zinazopeana ESOL katika mtaa wako. Hizi zinaweza kuwa:

→ Chuo cha Elimu ya Juu
→ Chuo cha Ngumbaru
→ Vyuo Vikuu
→ Mashirika ya kujitolea na ya Jamii
→ Vituo vya Learndirect kwenye mtandao wa intaneti
→ Mashirika ya mafunzo ya faragha

Kiingereza cha Biashara

Vyuo vingi vya Elimu ya Juu vinafunza mafunzo ya kiingereza cha Biashara, lakini inaweza ikawa utalipa. Afisi za agenti wa biashara, baraza la mitaa zinaweza kukusaidia kupata mahala pa kupata masomo haya.

(Kunaweza kupatikana kwa mashirika mengine ya mtaa kama vile; Taasisi ya Huduma kwa wakimbizi (Refugee Council) na taasisi ya Ushauri wa Mafunzo na Elimu kwa Wakimbizi (Refugee Education and Training Advisory Service (RETAS) zote zinatoa mafunzo ya kiingereza cha biashara, lakini ni lazima uangalie kama kuna mafunzo yanayotolewa karibu na unapoishi.)

→ Uliza usaidizi kutoka mtu yeyote anayeishi katika jamii yako ambaye anakifahamu vizuri kiingereza cha biashara.
→ Huduma za kutafsiri (unaweza kujaribu kwa baraza la mitaa au shirika la jamii) wanaweza kukutafsiria ama kukusaidia kutafsiri stakabadhi unazotumia katika biashara. Itabidi ulipie huduma hii.

© The Prince's Trust and the Refugee Council 2006

Kile unachoweza	Kile usichoweza
JIUNGE na darasa kama unaweza. Kama huwezi kutumia njia nyingi vivi hivi ziwezekanazo kuimarisha Kiingereza chako. Kiwango kizuri cha Kiingereza kitakusaidia kuwa huru zaidi kufuatilia nafasi nyingi za kufaulu katika biashara yako.	USITARAJIE kila mtu akusaidie huku tegemeo kutoka kwao likiwa muhimu, inafaa uweze kukagua ni nini haswa kinachoendelea katika kila sehemu ya biashara yako.

Unaweza kupata taarifa zaidi hapa:

- → Learndirect www.learndirect.co.uk
- → Chuo cha Elimu ya juu
- → Kituo Cha Kazi (Jobcentre Plus), wata kuelezea ambapo unaweza kupata usaidizi wa ESOL www.jobcentreplus.gov.uk
- → Kitengo cha Mashauri na Maongozi Kwa Wakimbizi (Refugee Advice and Guidance Unit) inatoa ushauri na mafunzo kwa wakimbizi www.londonmet.ac.uk/ragu/home.cfm
- → RETAS inatoa mafunzo kwa watendaji wa biashara www.education-action.org
- → Baraza la Wakimbizi (Refugee Council) linatoa mafunzo ya Kiingereza cha kibiashara www.refugee-council.org.uk
- → Maktaba iliyo karibu nawe
- → Halmashauri ya Ushauri kwa Wananchi (Citizens Advice Bureau) www.citizensadvice.org.uk
- → Idara ya Masomo katika Baraza lako (Education Department)

Hatua 5: Pata mafundisho kuhusu kufanya biashara

Kuna nafasi kadha za kupata masomo ya kukusaidia kuanza biashara hapa Uingereza. Masomo haya yatashughulikia:

- → Kukufahamisha kuhusu nafasi za kujiajiri hapa Uingereza
- → Kukupatia nafasi ya kugundua maarifa uliyonayo
- → Kukueleza jinsi ya kuanzisha biashara yako
- → Muhtasari wa jinsi ya kujitayarisha kabla ya kuanza biashara yako
- → Usaidizi wa kuandika mpango wako wa biashara
- → Utapa kujua kuhusu Ushuru, VAT na nambari Bima ya taifa (National Insurance)
- → Pia utapata nafasi ya kukutana na kutambua wengine wanao anzisha biashara

Kuna uwezakano kwamba utahitaji kulipa. Mafunzo haya yatakuwa ni akiba nzuri ya maarifa, ukiangalia kwamba una pungufu fulani katika ujuzi ulio nao kabla ya kuanza bashara yako. Mashirika kadhaa yanatoa mafunzo ya biashara haswa kwa wakimbizi. Mashirika au ofisi za ajenti wa wakimbizi wanaweza kujua kitu fulani ambacho kiko karibu na eneo lako.

© The Prince's Trust and the Refugee Council 2006

Unaweza kupata taarifa zaidi hapa:

- → Ofisi za maajenti ambao wanatoa malezi ya kibiashara, yako kwenye hifadhi ya Mwana Mfalme (Prince's trust) orodha ya muongozo wa kuanzisha biashara No. 12 – Nafasi za Usaidizi.
- → RETAS wanaendesha masomo ya kibiashara na pia kutoa usaidizi kwa wakimbizi na wale wanaosaka kimbilio wasio na kazi lakini wako makini), a) kuanzisha biashara yao wenyewe, na b) kuingia katika ushirikiano na vyama vya ushirika, (sana sana katika eneo la London). www.education-action.org / na RETAS.
- → Baraza la Wakimbizi (Refugee Council) linatoa mafunzo kuhusu , " Kuendeleza wakimbizi kuingia katika Soko la Wafanyikazi Uingereza" www.refugeecouncil.org.uk
- → Mtandao wa amali kwa Jamii (Community Action Network) unatoa mafunzo ya biashara kwa wakimbizi walio Uingereza www.can-online.org
- → Muungano biasharani (Business Link) ni shirika la uma ambalo linapatiana mawaidha ya kibiashara kwa biashara ndogo na za wastani. Linatekeleza shughuli zake kupitia vikundi katika mtaa. Pata kujua kikundi kilicho karibu nawe www.businesslink.gov.uk
- → Shirika la Wakimbizi la Umoja wa Mataifa (United Nations Refugee Agency) (UNHCR) ikipitia mtando wa Wakimbizi kwenye intaneti ('Refugees Online') inaweza kuwa ya usaidizi www.refugeesonline.org.uk

Hatua 6: Jitolee kufanya kazi katika biashara ndogo iliyo karibu nawe au pia jitolee kusadia katika Jamii

Kujitolea ni kufanya kazi bila malipo. Fikiria vile unaweza kujitolea kufanya kazi katika biashara iliyokaribu nawe au katika mradi wa jamii. Hii inaweza kukusaidia:

→ Kupata ujuzi kuhusu biashara ambayo ungependa kuanzisha.
→ Kuimarisha ujuzi fulani
→ Nafasi nzuri kufanya mazoezi ya kiingereza chako
→ Itaimarisha CV yako kwa kuonyesha kwamba una ujuzi wa kufanya kazi hapa Uingereza
→ Utapata kumbukumbu. Wenzako pale kazini watafurahia kukuandikia barua hii

Unaweza kujitolea, kama unasaka kimbilio cha hifadhi na bado unangoja kupata ruhusa ya kubaki.

Jinsi ya Kupata nafasi za kujitolea

→ Uliza mtu unayejua ambaye ana biashara yake kama unaweza kujitolea kusadia bila malipo
→ Fikiria kuhusu biashara unayotaka kuanzisha na shirikiana na biashara iliyo sawa na yako Karibu nawe
→ Tafuta miradi inayo shughulikia Jamii iliyo Karibu nawe na ujitolee katika miradi ile

© The Prince's Trust and the Refugee Council 2006

Unaweza kupata taarifa zaidi hapa:

- → Kituo cha Kimataifa cha watu wanaojitolea (National Centre for Volunteering) www.volunteering.org.uk
- → Reach www.volwork.org.uk
- → Kundi la amali kwa Wakimbizi (Refugee Action) www.refugee-action.org.uk
- → Baraza la Wakimbizi (Refugee Council) www.refugeecouncil.org.uk
- → RETAS www.education-action.org
- → Timebank www.timebank.org
- → Usitawi kwa waliojitolea nchini Uingereza (Volunteer Development England) www.vde.org.uk
- → The Prince's Trust www.princestrust.org.uk

Hatua 7: Panga vile watoto wako watachungwa ukiwa kwenye biashara au masomo

Kama unawachunga watoto wako wewe mwenyewe na pia una shughulikia kuanzisha biashara yako, utapenda kupanga malezi ya watoto ambayo itakupa imani na utakayokifurahia.

Baadhi ya mawaidha ni:

→ Marafiki au familia yako wanaoweza kuwaangalia watoto wako.

→ Wasaidizi wa kuchunga watoto Karibu nawe. Kama una wasiwasi kuwaacha watoto wako na watu usio wafahamu, unaweza kuwatumia yaya ambao wamesajiliwa. Yaya waliosajiliwa :
  - Wemehitimu kuwachunga watoto
  - Wana hakikisha kwamba kuna mazingira salama kwa watoto wako maanake wanapasiwa kuchukua madaraka
  - Huwa wanafurahia kama utachukua muda kupata kuwajua zaidi na vile ambavyo wanamchunga mtoto wako.

→ Serikali itatoa msaada wa kiasi, kama vile utaweza kupata msaada wa kifedha ili kulipia kuchungwa kwa mtoto wako kwa kupitia mpango wa Serikali wa kudai ushuru unaolipa ukifanya kazi (Working Tax Credit). Angalia sehemu ya chini kwa taarifa zaidi ya kupata anwani na nambari za simu.

→ Unaweza pia kuuliza mawaidha kutoka agenti spesheli kama vile Familia za Mzazi Mmoja (One Parent Families) wanao endesha Lone Parent Helpline. Nambari ya simu – 0800 0185 026.

→ Unaposaka usaidizi wa kuanza (hatua 9) uliza zaidi juu ya habari hii.

© The Prince's Trust and the Refugee Council 2006

Unaweza kupata taarifa zaidi hapa:

- → Nambari ya simu ya msaada wa ushuru wa kukopa kwa mfanyikazi (Working Tax Credit Helpline) (England Wales Scotland) 0845 300 3900/Northern Ireland 0845 603 2000
- → Sure Start ; huu ni mpango wa serikali wa kumpa kila mtoto mwanzo mwema. Pia katika mradi huu utapata taarifa zaidi kuhusu mfumo wa kulea mtoto Uingereza na jinsi ya kupata usaidizi wa kifedha www.surestart.gov.uk or www.childcarelink.gov.uk
- → Familia za Mzazi Mmoja (One Parent Families) wanajihusu kusaidia wazazi pweke www.helpdesk.oneparentfamilies.org.uk (England and Wales) www.opfs.org.uk (Scotland)
- → Gingerbread inaendesha wavu wa familia za mzazi mmoja www.gingerbread.org.uk
- → Hifadhi ya Kuwachunga Watoto Wadogo (Daycare Trust) ni shirika la taifa la kuwachunga watoto. Anwani yao katika mtandao wa intaneti itakusaidia kujua zaidi kuhusu kumlea mtoto www.daycaretrust.org.uk
- → Chama cha Taifa cha Kuwalea watoto (National Day Nurseries Association) (NDNA) ni chama cha taifa ambacho kinalenga kuimarisha elimu na maendeleo ya watoto wakiwa wachanga www.ndna.org.uk
- → Chama cha taifa cha kuwachunga watoto (The National Childminding Association) (NCMA) ni chama cha taifa na pia kimesajiliwa na shirika la wachunga watoto la Uingereza na Wales www.ncma.org.uk
- → Vuguvugu la Shule za Watoto Wadogo (The Pre-school Learning Alliance) ni chama cha usaidizi katika masomo kinacho angazia mahitaji ya watoto wakiwa wachanga www.pre-school.org.uk

Hatua 8: Panga matumizi ya pesa zako

Akaunti za Benki
Kama unataka kufungua akaunti, utahitaji kuwa na kitambulisho chako. Benki itahitaji kuona Kibali cha usafiri (passport), leseni ya kuendesha gari, au risiti ya kulipia stima ama maji.

Kama huna stakabadhi hizi uliza kama benki itaweza kukubali stakabadhi zingine za kujitambulisha kama vile Barua rasmi ya kubaki nchini (Leave to Remain) au stakabadhi zingine kutoka afisi ya Ndani (Home Office).

Itakuwa rahisi kwako kufungua **akaunti ya kawaida** (basic bank account) badala ya **akaunti ya desturi** (current bank account). Kwa akaunti hizi, ya kawaida na ya desturi unaweza:

→ Kuwa na kadi ya pesa unayoweza kutumia katika chombo cha kutoa pesa
→ Kuweka pesa ndani na kulipia gharama za maji, stima na kadhalika
→ LAKINI unaweza kupata deni ('overdraft') tu uliyokubaliana, ukitumia akaunti ya desturi

Kuchukua deni (Overdraft) inakuwezesha kutumia pesa nyingi kuliko zile ukonazo kwa akaunti. (Benki inakukopesha). Benki itakutoza kuichukua deni hii na wakati mwingine kukutoza gharama zingine zaidi kuhusiana na deni ile. (Financial Services Authority (FSA), 2006).

Ukiwa na akaunti ya **kawaida** (basic account), benki huenda haitakuruhusu kuchukua deni (overdraw)zaidi ya £10. Benki itataka kuangalia historia yako ya kukopa na itatumia habari hii kuamua kama watakupa akaunti ya **desturi** (current bank account) ama mkopo. Wataangalia:

→ Akaunti tofauti ambazo umewahi kuwa nazo
→ Madeni yote ambayo unaweza kuwa nayo

© The Prince's Trust and the Refugee Council 2006

Sio kila wakati benki zitaweza kupata historia ya akaunti zako kwa sababu umetoka kwenye nchi nyingine. Kwa hiyo itaweza kuwa vigumu kiasi kufungua akaunti ya **desturi**. Benki ikikataa maombi yako, basi ulizia akaunti ya **kawaida**.

Ukiwa na shida ukifungua akaunti, wasiliana na balozi la wakimbizi iliyo karibu, ama afisi ya mawaidha kwa wananchi (Citizens Advice Bureau) walio fanya kazi nyingi kuhusu jambo hili. Mahala pengine pa usaidizi ziko ukurasa ujao.

Dini ya Islam na Fedha
Ukiwa wewe ni Muislamu, basi itakuwa jambo la busara kufikiria juu ya "Riba" kabla ya kuanzisha akaunti yako. Riba ni kulipa au kupokea ada. Hii haikubaliki katika Shariah manake ni kujiweka kwenye hatari ya "gharar".

Unaweza kusuluhisha vipi hali hii?
→ Pata kutafuta ushauri kutoka kwa marafiki, familia na wengineo katika jamii, ambao wameanzisha biashara zao
→ Kuna benki na mashirika ambayo yanaweza kukusaidia kwa sababu wanafanya shughuli zao kulingana na Shariah

Benki na Mashirika yanayofuata Shariah ni kama:

Benki ya Waislamu ya Uingereza (Islamic Bank of Britain) inafuata Shariah.

HSBC ambao walianzisha kitengo cha Amanah (Amanah division) mwaka wa 2003 ili kuwapa Waislamu njia ya kukopa pesa za kununua nyumba na kuwa na akaunti za kibinafsi. Kwa sasa inashughulikia kuona vile wanavyoweza kuwasaidia Waislamu watendaji katika biashara. Benki ya Islamic Bank of Britain imetimiza matakwa ya Shariah.

Hifadhi ya Mwana Mfalme (The Prince's Trust) imemuuliza mtalaam wa Shariah awape mawaidha juu kulipa mikopo kutoka kwa Hifadhi hii inayotolewa kwa vijana Waislamu. Imepitishwa kwamba gharama zinazotozwa na hifadhi hii ziwe tu ni gharama za kikazi na sio riba.

Unaweza kupata taarifa zaidi hapa:

- → Mtandao wa intaneti wa Idara inayo shughulikia huduma za Fedha (Financial Services Authority) inatoa mawaidha kuhusu akaunti za kawaida www.fsa.gov.uk
- → Afisi ya mawaidha kwa wananchi (Citizens Advice Bureau) www.citizensadvice.org.uk
- → Islamic Bank of Britain www.islamic-bank.com
- → Kupata taarifa zaidi kuhusu HSBC Amanah angalia kwenye anwani yao ya intaneti www.hsbcamanah.com
- → Muongozo wa 2 Kuanzisha Biashara Yako (Start up Guide 2) una taarifa muhimu ya vile unaweza kupata mkopo wa biashara www.refugeesintobusiness.org.uk/guide
- → Muongozo wa 12 Njia za Usaidizi (Start up Guide 12) una orodha ya mashirika yanayotoa usaidizi wa kifedha www.refugeesintobusiness.org.uk/guide

© The Prince's Trust and the Refugee Council 2006

Hatua 9: Pata usaidizi kutoka kwa watalamu katika kuanzisha baishara yako

Kuna mashirika mengi huko Uingereza zinazo weza kukupa msaada unapojitayarisha kuanza biashara yako, mara nyingi wakipeana washauri na waongozi wataokupa msaada moja kwa moja. Ushauri kutoka kwa mtaalam wa biashara, ni njia moja wapo unaoweza kukusaidia kujua kama kuendesha biashara inakufaa na pia vile kuiendesha.

Mashirika ya Kuanzisha Biashara
Kuna mashirika ya kiserakali, ya kibinafsi na vyama vya kujitolea yanayo peana:

→ Ushauri na muongozo wa jinsi ya kuanzisha biashara yako
→ Mafunzo ya utendaji biashara
→ Usaidizi wa kuandika mpango wako wa biashara
→ Taarifa kuhusu mikutano ya watendaji biashara

Huduma kadhaa ni za bure, zingine utapata kulipa. Angalia lile lapatikana karibu nawe.

Mshauri wa Kibiashara
Mshauri wa kibiashara hukupa mawaidha kwa mfano juu ya vile utakavyoandika mpango wako wa biashara, mambo ya sheria na hata kuhusu matumizi bora ya fedha. Washauri wengi wemehitimu kwenye masomo ya biashara na wana ujuzi mwingi katika biashara. Pia wanaweza kukusaidia kutatua shida fulani na kukupa suluhisho kwa matatizo magumu. Mshauri anaweza kusaidia kwa muda au wakati unapomhitaji tu. Inawezekana utalipa huduma hii. Unaweza kupata muongozo wa jinsi ya kumchagua mshauri wa biashara yako katika mtandao wa intaneti wa Muungano katika Biashara (Business Link).

Tofauti kati ya mshauri wa biashara na mwongozi katika biashara
Mshauri wa biashara ni mtaalam atayekupa ushauri maalum. Mwongozi katika biashara sana sana ni mtu aliyejitolea na hupeana mawaidha ya kawaida kuhusu biashara na kutoa hoja kuhusu mawazo na shida zilizo katika biashara.

Mwongozi katika biashara

Mwanabiashara huyu hupeana mara kwa mara mawaidha ya kibiashara kwa mtu anaye anzisha biashara. Lengo la mwongozi katika biashara, ni kuweza kukusaidia kuanza biashara itayoweza kufululiza na itakayo fanikiwa. Waongozi katika biashara sana sana wana ujuzi mzuri tena imara katika biashara.

Kwa kawaida huyu mwanabiashara hupeana msaada wa siri kwa muda uliokubaliwa, sana sana huwa ni kama muda wa miezi sita hadi miaka miwili.

- → Mashirika mengine yanatoa usaidizi wa kuanzisha biashara pamoja na kutoa waongozi katika biashara. Agiza habari zote kuhusu huduma hii
- → Wafanyi biashara hawa wenye ujuzi hutoa mawaidha ya bure kwa kujitolea tu. Hakikisha kwamba hivyo ni kweli kabla ya kuuliza mawaidha

© The Prince's Trust and the Refugee Council 2006

Unaweza kupata taarifa zaidi hapa:

Usaidizi wa kuanzisha biashara yako

→ Muongozo wa 12 Njia za Usaidizi (Start-up Guide 12 - Sources of Help) lina orodha ya mashirika ambayo yanaweza kukusaidia www.refugeesintobusiness.org.uk/guide

Huduma kwa vikundi maalum

→ Hifadhi ya Mwana Mfalme (The Prince's Trust) husaidia vijana kati ya miaka 18 – 30 ambao hawana kazi kuanzisha biashara zao www.princes-trust.org.uk

→ Shell LiveWire huwapa motisha vijana kati ya miaka 16 – 30 kuanza na kujenga biashara zao wenyewe www.shell-livewire.org

→ The Prime Initiative ni shirika la kitaifa ambalo linashughulikia tu kuwasaidia watu walio na miaka 50 au zaidi kuanzisha biashara www.primeinitiative.org.uk

Huduma zinatolewa kwa wote

→ Shirika la Muungano katika Biashara (Business Links) www.businesslink.gov.uk.

→ Ofisi za majenti wa Watendaji Biashara (Local Enterprise Agencies) (LEAs) www.nfea.com

→ Chama Cha Wafanyi biashara (Chamber of Commerce) www.britishchambers.org.uk

→ Mradi wa Kujitolea na Uongozi kwenye biashara (Business Volunteer Mentoring (BVM) Programme) www.bvm.org.uk

Hatua 10: Mahala pengine pa kupata usaidizi

Familia yako, marafiki na jamii wanaweza kuwa mahala nzuri ya usaidizi. Wanajua uwezo na udhaifu wako vizuri zaidi kuliko mtu mwingine yule. Usaidizi ambao watakupa pamoja na ule wa mtaalam au Mshauri wako utakuwezesha kufanya uamuzi kama utaanzisha biashara yako na jinsi utakavyo iendeleza.

Maria na Luisa, ni wakimbizi kutoka Angola
Maria na Luisa ni marafiki. Wote wawili wametoka Angola na kwa sasa wanaishi eneo la Manchester. Maria angependa kufungua mkahawa na wanashauriana ni nini atakalofanya…

Luisa: Hili ni wazo zuri sana Maria! Chakula chako huwa murwa kila wakati! Pia unajua kukaa na watu vizuri. Eneo hili linahitaji sana kuwa na mkahawa. Itakuwa vizuri kuwa na mahala ambapo marafiki wetu wanaweza kukutana haswa wale kina mama wachanga.

Maria: Je, unajua pahali ambapo naweza kupata pesa za kuanzisha biashara hii?

Luisa: Nina binamu yangu, James, ambaye alianzisha biashara labda anaweza kukusaidia.

Maria: Hilo ni wazo zuri, nitamuuliza mara moja.

Luisa: Nina wazo lingine Maria: wiki mbili zilizopita nilialikwa kwa chakula cha kutwa na rafiki yangu Susan. Tulienda kwa mkahawa mashuhuri sana wa Afro – Caribbean kule Old Trafford. Mkahawa huo unamilikiwa na shangazi na ami yake Susan. Mbona usiwaulize kama unaweza kufanya kazi pale bila malipo kwa majuma kadhaa ili upate kujua kama unaweza kufanya biashara ya mkahawa au la? Ninaweza kukujulisha kwa Susan.

Maria: Kweli hilo ni wazo zuri zaidi! Labda watakubali nipike vyakula vya Angola na kuona kama wateja watavipenda au la. Asante sana kwa ushauri wako Luisa. Nimefurahia kuongea nawe.

© The Prince's Trust and the Refugee Council 2006

Kuongea na marafiki, familia na watu wengine katika jamii itakusaidia:

- → **Kujua uwezo wako:** Luisa anamfahamu Maria vizuri sana. Jinsi Luisa alivyomwitikia Maria, ilimsaidia Maria kujua kama ana maarifa yanayohitajika.
- → **Kugundua nafasi ya kujitolea:** Kufanya kazi katika mkahawa itamsadia Maria kuelewa kile kinachohitajika kufanya biashara yake ya Mkahawa.
- → **Ongea kuhusu wazo lako la biashara:** kwa kuongea kuhusu wazo lake na Luisa , Maria alipata kujua kama mkahawa unahitajika katika eneo lao.
- → **Pata kujua pahala pa kupata usaidizi wa biashara:** Maria anaweza kumuuliza James vile alivyoanzisha biashara yake na vile alipata mkopo wake. Hii ni njia nzuri ya kupata usaidizi wa kuanzisha biashara yake.
- → **Kutambua muongozi katika biashara:** Maria anaweza kumuuliza James, au Shemejie na Mjombake Susan kama mmoja wao angefurahia kumsaidia kwa njia ya kuongoza kwani wao wameshaanza biashara zao.

Kile unachoweza	Kile usichoweza
ANDIKA usaidizi wote ambao unaweza kupata kutoka kwa familia, marafiki na jamii. Pia wasiliana na mashirika ya kuanzisha biashara na uliza kama wana mshuari wa biashara.	USIWATEGEMEE sana marafiki, familia na jamii. Hawataweza kuwa na taarifa zote kamili na pia hawatalaumiwa jambo linapoenda kuharibika. Ni muhimu kupata mawaidha na usaidizi wa wataalam ili kuzuia shida zinazoweza kutokea au kusuluhisha matatizo magumu.

Taarifa hii imeandikwa na Hifadhi ya Mwana Mfalme (The Prince's Trust) kwa niaba ya Baraza la Wakimbizi (Refugee Council) na mwanzo tu wa shughuli ambazo zimeanzishwa. Ni muhimu kupata mawaidha ya kiwakili na kifedha ya kibinafsi. Hakuna laumu lolote limekwa juu ya mchapishaji wa taarifa hii. Hifadhi ya Mwana Mfalme na Baraza la Wakimbizi halikubali kulaumiwa kuhusiana na ukamilifu wa taarifa zilizochapishwa hapa.

© The Prince's Trust and the Refugee Council 2006

Cover design by Morse-Brown Design
© The Prince's Trust and the Refugee Council 2006